

# ZIJUE KANUNI ZA KILIMO BORA CHA ZABIBU

DR. A.W.MALEKANI

CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO
MAKTABA YA TAIFA YA SOKOINE YA KILIMO
GHALA LA MACHAPISHO YA MKULIMA

Adobe Spark

## Yaliyomo

ZIJUE KANUNI ZA KILIMO BORA CHA ZABIBU ............................ Error! Bookmark not defined.
UTANGULIZI ........ 3
1:0 HISTORIA YA KILIMO CHA ZABIBU KWA UFUPI ........ 3
1.1 Ukweli kuhusu kilimo cha Zabibu ........ 4
1.2 Maeneo yanayolimwa Zabibu mkoani Dodoma ........ 4
2.0 HATUA KUMI ZA KUANGALIA KABLA HUJAANZISHA SHAMBA LA ZABIBU ........ 4
2.1 AINA YA ZABIBU ........ 6
2.2 HALI YA HEWA ........ 6
4. HATUA ZA KUFUATA WAKATI WA UANZISHWAJI WA SHAMBA LA ZABIBU ........ 6
Kuchukua sampuli ya udongo mahali unapotaka kuanzisha au kupanda zabibu ........ 7
Hatua inazopitia mmea wa mzabibu toka kukatiwa mpaka kuzaa matunda yenye ubora ........ 14
Ugonjwa wa Kinyaushi (Dampingoff) ........ 15
Ugonjwa wa Ubwiri Poda (Powderymildew) ........ 16
Ukungu wa kuchelewa (Lateblight) ........ 16
MWISHO ........ 19
Bibliografia ........ 20

## UTANGULIZI

Kitabu hiki kinatoa mwongozo wa mbinu bora za uzalishaji wa Zabibu kwa mkulima wa kawaida, pia tumetumia lugha rahisi ili kumuwezesha mkulima kuelewa kwa urahisi, pia kimetumia michoro mingi ili kumsaidia mkulima kuona kwa vitendo, na pia kimetumia mazingira halisi ya Wakulima wa Zabibu mkoani Dodoma.

Jitihada nyingi zimefanyika ili kuhakikisha Wakulima wa Zabibu mkoani Dodoma wanalima kisasa zaidi ili kujihakikishia mavuno bora na ya uhakika kipindi cha msimu wa mavuno.

Kutokana na utafiti uliofanyika na Taasisi mbalimbali inaonyesha kuwa asilimia kubwa ya Wakulima wa Zabibu mkoani Dodoma wanalima kwa kutumia uzoefu tu na si kitaalamu kama inavyotakiwa, hii inapelekea Wakulima wengi kutumia gharama kubwa katika uzalishaji wa zao hili kwa kuwa wengi wao wanatumia uzoefu na si utaalamu, hivyo kupelekea Wakulima kupata kipato kidogo ambacho hakilingani na uwekezezaji walioweka.

Hivyo kitabu hiki kitaainisha mbinu zote za msingi katika uzalishaji wa Zabibu ili kumpunguzia mkulima gharama za uzalishaji, na pia kuendesha kilimo kibiashara zaidi.

Nimatumaini yangu kuwa kama Wakulima watazifuata mbinu hizi wataongeza uzalishaji wa zao hili na hivyo kuwaongezea kipato zaidi.

## 1:0 HISTORIA YA KILIMO CHA ZABIBU KWA UFUPI

Kilimo cha Zabibu mkoani Dodoma kina historia ndefu, ambapo kwenye miaka ya 1950 na mwaka 1974 chini ya usaidizi wa Bihawana misheni, serikali ya Tanzania wakati huo ikishirikiana na serikali ya China ilianzisha kituo cha kilimo cha Bihawana Farmers Training Center (BFTC) kwa ajili ya kufundisha Wakulima juu ya kilimo cha Zabibu na mazao mengine.

Wakulima wengi walijifunza mbinu mbalimbali juu ya kilimo cha Zabibu na wengi wao walianzisha mashamba ya Zabibu. Na katika miaka ya 1990 kilianzishwa kiwanda cha mvinyo cha DOWICO, kiwanda hiki kilisababisha Wakulima wengi waingie kwenye kilimo cha Zabibu.

Katika miaka hiyo ya 1990 viwanda vya mvinyo viliongezeka na Wakulima wengi wakaanza kuanzisha mashamba ya Zabibu ili kuvilisha viwanda hivyo.

Dodoma ndio mkoa pekee unaolima Zabibu kwa wingi nchini Tanzania na hata kwa Afrika Mashariki ndio mkoa wenye utajiri mkubwa wa zao hili. Hii pekee ni fursa kwa wananchi wa Dodoma katika kulitilia mkazo zao hili ili liweze kuinua uchumi wa wananchi wa mkoa huu.

Kijitabu hiki cha kilimo bora cha Zabibu kimeeleza kwa undani juu ya mbinu zote za kilimo cha Zabibu kuanzia kujua aina ya udongo, uandaaji wa shamba, maji, magonjwa, uvunaji, aina za Zabibu n.k napia kimeangazia muelekeo wa kilimo cha Zabibu kibiashara zaidi.

### 1.1 Ukweli kuhusu kilimo cha Zabibu

Katika kiini chake kilimo ni utatuzi wa changamoto mbalimbali, kwahiyo kama hutajiweka kama mtatuzi wa changamoto hizo ni bora uachane na kilimo. Kila siku shamba la Zabibu litakuletea changamoto mbali mbali ambazo itakubidi uzikabili:

Je, unaweza kipindi cha mvua kukabiliana na magugu, unaweza ukapalilia leo baada ya siku tatu yakaota mengine, hali kadhalika kipindi cha mavuno kinapokaribia kuna changamoto ya ndege wanaokuja kuharibu Zabibu na hao pia inabidi ukabiliane nao, Je uko tayari? Swali la msingi hapa ni kwa namna gani utalima Zabibu katika vipindi vyote vya masika, kiangazi n.k katika vipindi vyote hivi kuna magonjwa kulingana na hali ya hewa ya kipindi husika.

### 1.2 Maeneo yanayolimwa Zabibu mkoani Dodoma

Hali ya hewa ya Dodoma inaruhusu zao hili kustawi katika maeneo mengi mkoani hapo, baadhi ya maeneo yanayolimwa Zabibu ni Mpunguzi, Mbabala, Hombolo, Chamwino, Bahi, Mvumi, Msalato na Gawaye.

Kwa asilimia kubwa maeneo haya yanategemea mvua na kwa baadhi ya maeneo wanatumia mifumo mbalimbali ya umwagiliaji mfano Hombolo wanatumia mifereji inayopitisha maji kutoka bwawa la Hombolo, Chamwino wanatumia umwagiliaji wa matone.

## 2.0 HATUA KUMI ZA KUANGALIA KABLA HUJAANZISHA SHAMBA LA ZABIBU

Kumekua na wimbi kubwa kwa watu wanaofanya kazi za maofisini kuingia kwenye kilimo hiki hasa wakijua kua kilimo hiki kina tija katika kujikwamua kiuchumi, na hii imepelekea hata wale wakulima wazoefu na wenyewe kuongeza mashamba yao, huku wakiamini kuwa ipo siku zao hili litarudisha heshima yake ya miaka ya tisini, kwakua sasa Zabibu inalimwa na watu wa kada tofauti tofauti. Hivyo basi kabla hujaamua kuingia kwenye kilimo hiki au kupanua shamba lako hebu jaribu kupitia hatua hizi ndipo ufanye maamuzi sahihi.

1. Kwanza unatakiwa uangalie kuwa unalenga soko lipi, je ni kwa wenye viwanda? Au wanunuzi wadogo wadogo? Kama ni kwa wenye viwanda inabidi ujaribu kuongea nao kwanza uone mtazamo wao na ni aina ipi ya Zabibu wanazihitaji.

Ni wazo zuri pia kama utapata mawasiliano ya uhakika na wenye viwanda ikibidi kama watakuhakikishia kuingia mkataba nao mara utakapoanza uzalishaji.

2. Pili inabidi ujue nini unakifanya, hapa yaani ujuzi wa zao hili, wengi wa Wakulima wanaolima zao hili kwasasa hawana utaalamu wengi wao wanatumia uzoefu tu. Si kwamba wanafanya vibaya ni kitu kizuri kutumia uzoefu lakini ukiongeza na ujuzi kidogo inakua ni kitu kizuri zaidi, maana utajua nini unafanya katika kilimo hiki.

3. Tatu fanya utafiti binafsi kwa kuongea na Wakulima wazoefu ili kujua ni aina gani ya Zabibu inastawi katika eneo husika, pia kuna mabwana shamba ambao wana utalaamu juu ya kilimo hiki cha Zabibu nenda kaongee nao uone wanakushauri nini. Pia ni vyema ukazalisha Zabibu ambazo wenye viwanda vya mvinyo wanazihitaji wao ni soko la uhakika.

4. Nne kama mipango pia nikuanzisha kiwanda cha mvinyo ili Zabibu utakazolima uzipeleke kiwandani kwako. Nivyema ukafanya utafiti juu ya Masoko ya mvinyo utakaotengeneza, ujue wateja wako ni kina nani wanapendelea mvinyo wa aina gani n.k

5. Uwe na mtaji wa kutosha utakaokuwezesha kuishi kwa miaka mitatu hadi mitano bila kutegemea kipato chochote kutoka kwenye shamba lako la Zabibu, maana Zabibu itaanza kukulipa kuanzia mwaka wa tatu na kuendelea.

6. Sita hakikisha unaanzisha shamba kwenye udongo sahihi unaoendana na uzalishaji wa Zabibu, udongo ndio kitu cha msingi kabisa kuzingatia kabla hujaamua kuanzisha shamba la Zabibu.

7. Saba anza na ekari chache hii itakusaidia uendelee kujifunza taratibu juu ya kilimo hiki kwa vitendo huku akili yako ikiwa imetulia, usianze na uwekezaji mkubwa maana utakupa changamoto kwa kuwa ndio mara yako ya kwanza kuanza kilimo hiki.

8. Nane, tafuta mkulima mzuri na mzoefu mwenye shamba zuri la Zabibu, au jiunge na vyama vya Wakulima wa Zabibu kama UWAZAMAM, MBABALA, GAWAYE N.K hapa utapata fursa ya kujifunza kwa vitendo namna wenzio wanavyolima Zabibu na namna wanavyokabiliana na changamoto mbalimbali za zao hili.

9. Jaribu kujifunza namna bora ya ukatiaji wa Zabibu, katika kilimo hiki cha Zabibu ukatiaji ndio kiini cha uzao wa Zabibu, ukikosea katika ukatiaji unaweza usipate mazao kwa msimu mzima. Hivyo ni muhimu ukajifunza namna bora ya ukatiaji wa mizabibu. Utaelewa kwa kina juu ya ukatiaji katika sura zinazofuata za kitabu hiki.

10. Kumi, uwe na mtazamo wa kulima kibiashara zaidi, usilime Zabibu kwa mazoea, lima zao hili huku ukiamini kuwa hii ni kazi yako usilime kama kazi ya ziada tu. Ongeza juhudi na maarifa katika kilimo hiki.

Nimeamua kukuwekea hatua hizo kumi za kufuata kabla hujaanzisha shamba la Zabibu, hata kama tayari umeanzisha shamba la Zabibu jaribu kuzipitia hatua hizo uone kama ulizipitia au la,japo nimatumaini yangu kuwa kuna baadhi walizipitia hata kama sio zote.

## 2.1 AINA YA ZABIBU

Kwa ujumla kuna aina tatu za Zabibu ambazo ni Zabibu za mvinyo, Zabibu za mezani na Zabibu za kukausha ambazo zote zinazalishwa mkoani Dodoma. Zabibu zinazozalishwa kwa wingi mkoani Dodoma ni mvinyo zikifuatiwa na za mezani.

Aina zote hizo zilizotajwa hapo juu zimegawanyika katika makundi tofauti tofauti mfano Zabibu za mvinyo zimegawanyika katika makundi mawili ambapo kuna Zabibu nyekundu maalumu kwa ajili ya kutengenezea mvinyo mwekundu na kuna Zabibu nyeupe kwa ajili ya kutengenezea mvinyo mweupe.

## 2.2 HALI YA HEWA

Zabibu haihitaji mvua nyingi, maeneo yenye mvua za wastani ndio yanafaa kwa kilimo cha Zabibu mfano Dodoma. Unaweza ukajiuliza kwanini Dodoma ni pakame lakini ndio wazalishaji wakubwa wazabibu Afrika mashariki! Ni kwamba ardhi ya Dodoma ina hifadhi maji kwa kipindi kirefu mfano kwa mvua zinazonyesha kuanzia Desemba mpaka Machi ambazo zinatosha kabisa kuhudumia mizabibu mpaka mwezi wa Julai kwa mavuno ya kiangazi.

Hali hii ya Dodoma ndio inayofanya Zabibu yake kuwa bora kuliko sehemu yoyote ile Afrika Mashariki, zina kiwango kikubwa cha sukari, pia unaweza ukazihifadhi kwa muda mrefu kidogo, zina ganda gumu ukilinganisha na Zabibu za sehem nyingine.

# 4. HATUA ZA KUFUATA WAKATI WA UANZISHWAJI WA SHAMBA LA ZABIBU

Kabla ya kuanzisha shamba la Zabibu kuna hatua kumi za msingi za kuzifuata kwa mpangilio, ili kuweza kuleta tija katika uzalishaji wa Zabibu.

1. Kufanya utafiti juu ya aina ya udongo unaofaa katika uzalishaji wa Zabibu, katika utafiti niliofanya nimegundua Wakulima wengi hawafanyi utafiti juu ya udongo unaotakiwa katika uzalishaji wa Zabibu.

Udongo unaofaa kwa kilimo cha Zabibu kwa hali ya hewa ya Dodoma ni mchanganyiko wa mfinyanzi, kichanga na tifutifu, hata kama utapata mahali ambapo udongo huu wa mchanganyiko haupatikani itabidi uchimbe mitaro na unapochanganya mbolea itabidi uchanganye na aina hizo za udongo.

Moja ya faida ya aina hiyo ya udongo ni kuwa inasaidia mizizi ya mzabibu kujitawanya kwa nafasi, na pia hewa na maji vinapata nafasi kwa urahisi.

Picha: katika picha hii utaona jinsi mizizi ya Zabibu inavyojitawanya kwa nafasi kwa kua udongo huu Ulichanganywa vizuri na hivyo kuacha nafasi kwa mizizi kujitanua kwa urahisi.

## Kuchukua sampuli ya udongo mahali unapotaka kuanzisha au kupanda zabibu

•Vifaa vinavyohitajika ni jembe, panga, koleo, mifuko ya rambo, mifuko ya kaki na karatasi kubwa ya kuchanganyia sampuli za udongo.

•Angalia uoto wa asili wa shamba lako kama vile aina ya majani yaliyoota shambani.

•Gawanya shamba lako kulingana na uoto wa asili na umbo la shamba, kama vile sehemu ya juu na chini au sehemu yenye vichuguu na isiyo na vichuguu.


•Baada ya hapo mkulima achukue sampuli zake za udongo kwa mtindo wa zigizaga au herufi ya W. Mtindo huu unaoonyesha sehemu za kuchukua sampuli za udongo shambani kila penye nukta mkulima atachukua sampuli.

•Baada ya kuchukua udongo huo mkulima atapaswa kutoa tabaka la juu na kuchanganya udongo uliobaki.


•Mkulima atapaswa kuugawa udongo katika mafungu manne, sampuli namba 1, 2, 3 hadi namba 4. Anaweza kuamua kuchukua udongo namba 1 na namba 3 akauacha namba 2 na 4 na ataendelea kisha atachanganya zote kiufasaha na kuzigawa ili apate kiasi kisicho pungua kilo moja ambacho atapeleka maabara.


•Mkulima anatakiwa achukue angalau kilo moja kwa sampuli moja kwa ekari 2.5, na sampuli zaidi ya moja kwa eneo la zaidi ya ekari 2.5.

•Mkulima akisha chukua sampuli za udongo atapaswa kuandika juu ya mfuko wa kaki aliyofungashia jina la shamba au sehemu shamba lilipo, jina ya aliyechukua sampuli na tarehe aliyochukua.




**1.** Gawanya shamba lako kulingana na uoto wa asili au umbo. Chukua sampuli za udongo kwa mtindo wa zigizaga au herufi ya W.







2. Chukua sampuli kwa upana na kina kinachotakikana

2.1 Acha udongo wa juu chukua udongo wa chini





3. Changanya udongo kutoka kwa sehemu tofauti za shamba na hakikisha unacho kiasi kisicho pungua kilo moja.




4. Andika jina la shamba, sehemu shamba iliyopo, tarehe ya kuchukua sampuli, aliyechukua sampuli na tarehe na kuipeleka kwenye maabara ya kupima udongo.

**Picha namba 2:** Namna ya kuchukua sampli ya udongo kwenye shamba la kupanda Zabibu

Angalizo: Sampuli ya udongo inachukuliwa kabla ya shamba kulimwa na likiwa halina unyevu mwingi. Mkulima anapaswa kuwasiliana na mtalaam wa udongo aliye karibu naye kwa msaada zaidi.

2. Kuandaa mitalo kufuatana uelekeo wa jua linapotokea, unapoandaa shamba la Zabibu inabidi mistari ya mitalo uchore kufuatana na jua linapochomoza, moja ya faida ya kuangalia uelekeo wa jua ni kwamba chakula cha mmea kinatengezwa kwa nguvu ya jua pia, hivyo inakupasa kuangalia kigezo hicho ili kuweza kupata mimea yenye afya na uwezo wa kuhimili mazao yatakayo zalishwa, Zabibu inahitaji jua la kutosha ili kuweza kuzalisha chakula cha kutosha kwa mimea yake. Chimba mitalo yako na uhakikishe angalau inapata jua kwa asilimia 80.

Mitaro ya Zabibu kufuatana na ulekeo wa jua, mashariki kwenda magharibi kufuatana na picha hii

3. Kuhakikisha unapata miche bora ya mizabibu, hapa kuna Wakulima wana vitalu vyao na kuna wengine wananunua kwa Wakulima binafsi au kwa taasisi zinazojishughulisha na Zabibu mfano Makutupora kituo cha utafiti. Miche bora ya Zabibu ndio itakayo kuwezesha kupata mazao ya uhakika mbeleni, na ndio maana inashauriwa Wakulima wanunue miche bora iliyoandaliwa kitaalam.

Wakulima wengi mkoani Dodoma wanategemea makato ya miche kutoka kwenye mashamba yao kitu ambacho sio sahihi sana maana kunakua na mzunguko mkubwa/mrefu uzao, na pia Wakulima wengi wanashindwa kuchagua makato yenye ubora na hii hupelekea kukosa mazao ya uhakika.

**Picha namba 2:** Makato ya Zabibu yaliyoandaliwa katika ubora wa hali ya juu, yakisubiri kuchipua






**Picha namba 3:** Muonekano wa kitalu cha Zabibu kilichoandaliwa vizuri

4. Kuanda mitalo kabla hujahamishia miche shambani, hii ni hatua muhimu na Wakulima wengi hushindwa katika hatua na kujikuta wanaharibu miche mingi shambani mara tu baada ya kuihamishia maana miche huungua kwa kuwa wanashindwa kuchanganya kwa wastani mzuri mbolea na mchanga, unashauriwa katika kila kilo moja ya ya mbolea/samadi unachanganya mchanga robo kilo, na baada ya kuchanganya unatakiwa ufukie mitaro yako kwa muda wa mwezi mmoja au miwili ili kuacha mbolea ioze vizuri na kuiacha ardhi ikiwa na rutuba ya kutosha, pia tunashauri Wakulima wanaoandaa mashamba/mitalo mipya kuiandaa kuanzia mwezi November ili mvua zitakazoanza desemba zikute umeshafukia mitalo yako vizuri na kuozesha mbolea kwa haraka zaidi.



**Picha namba 4:** Udongo uliochanganywa vizuri na samadi




**Picha namba 5**: **Mtaro iliyoandaliwa vizuri kwa nafasi kwa ajili ya upandaji Zabibu**

5. Kuhamishia miche kutoka kwenye kitalu na kuhamishia kwenye shamba lililoandaliwa vizuri, usije ukahamishia miche kwenye shamba ambalo halikuandaliwa vizuri maana itakugharimu hutapata matokeo mazuri baada ya muda kupita.

Kabla ya kuanza kuhamisha miche kwenye shamba inabidi uhakikishe kuna maji ya kutosha maana kila mche unatakiwa uwe kwenye unyevu ili kuzoea maisha mapya ya shambani.pia ni vyema Wakulima wazingatie nafasi kati ya mche na mche na mtaro na mtaro


Shamba liloandaliwa vizuri tayari kuhamisha miche, hapa ndipo miche hii itamalizia masiha yao hapa hivyo ni vyema eneo liandaiwe vizuri.

6. Baada ya miche ya Zabibu kuhamishiwa shambani katika hatua hii, mkulima inakupasa kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kuhakikisha hakuna mmea unaokufa ama kwa ukame au kuliwa na wadudu. uzoefu unaonesha kuwa Wakulima wengi wakishahamishia miche shambani wanajua washamaliza kazi, hivyo ni vyema kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kujua maendeleo ya miche yote.



**Picha namba 6:** Mmea wa mzabibu wenye afya nzuri na ambao unafuatiliwa kwa ukaribu sana

7. Baada ya miche kushika vizuri, itaanza kustawi na kuonesha dalili za kutambaa, hivyo basi hichi ni kipindi cha kuanza kuifundisha namna ya kutambaa kwa kutumia kamba na fito nyembamba.





**Picha namba 7**: Picha hizi zinaonesha ni namna gani unaweza kufundisha mmea wa Zabibu namna ya kutambaa kwenye wire na fito

8. Baada ya kuufundisha mmea wa Zabibu, kinachofuata ni ukatiaji wa mzabibu, katika hatua hii hapa ndipo unaundaa mmea wako kwa ajili ya uzao, bila kukatia huwezi kupata mazao.
vifaa vinavyotumika kwa ukatiaji ni kama mkasi, msumeno n.k.. kuna aina mbili za ukatiaji wa mizabibu ambapo kuna Dodoma cordon ambao utakuwezesha kupata mazao kwa misimu miwili, na southAfrican type of pruning (ukatiaji wa kia Afrika kusini) ambao utakuwezesha kupata mazao kwa msimu mmoja.



**Picha namba 8:** Vifaa vya ukatiaji




**Picha namba 9: Namna ya ukatiaji**

9. Hatua inayofuata ni uzaaji wa mizabibu iliyokatiwa vizuri, kama ulivyoona katika hatua namba nane kuwa ukatiaji ndio unaosababisha mzabibu kuzaa, na pia ubora wa matunda.

## Hatua inazopitia mmea wa mzabibu toka kukatiwa mpaka kuzaa matunda yenye ubora

10. Moja ya mambo ambayo yamekua ni changamoto kubwa wakulima wengi ni Wadudu na magonjwa ya mizabibu. Magonjwa pamoja na wadudu waharibifu wanaweza kuchangia kupata hasara hadi ya asilimia 100. Baada ya kuandaa shamba, kununua miche na kupanda miche yako, kazi kubwa inakua ni utunzaji wa mizabibu yako. zabibu ni moja ya mazao yanayopendelewa

sana na wadudu na magonjwa, hivyo inahitajika umakini wa hali ya juu sana. Kwanza tunachotakiwa kufahamu ni kwamba Zabibu inahitaji ufuatiliaji wa karibu sana.

Kuna vitu viwili hapa vinatakiwa kuwekwa sawa:

Kuna kinga dhidi ya mzabibu –ambapo kuna dawa kwa ajili ya kinga na Kuna kutibu mzabibu baada ya kupata ugonjwa-kuna dawa zake pia.

Kitu ambacho Wakulima wengi hawafuatilii ni kwamba anaweza kupiga dawa ya kinga kipindi ambacho mzabibu ushaingia ugonjwa au anaweza piga dawa ya ugonjwa wakati mzabibu hauna ugonjwa huo hivyo unakuta Wakulima wengi wanaingia hasara ya madawa bila sababu.

Kitu kingine cha kuzingatia hapa ni vipimo vya dawa juu ya ugonjwa husika na ukubwa wa shamba, kwa bahati nzuri dawa nyingi siku hizi zimeandikwa kwa lugha nyepesi juu ya matumizi ya dawa hizo na vipimo vyake viko wazi kabisa. Kama umeambiwa uchanganye kilo moja kwa lita mia tatu za maji unashauriwa ufanye hivyo au kama umeambiwa lita moja ni kwa shamba la ekari moja basi huna budi kufanya hivyo na si vinginevyo. Kuzidisha dozi au kupunguza dozi haitakiwi katika kilimo hiki.

## Ugonjwa wa Kinyaushi (Dampingoff)

Ugonjwa wa Kinyaushi husababishwa na vimelea vya ukungu jamii ya (Pythium, Rhizoctoniasolani, Phytophthoraspp na Sclerotium). Ukungu huu au vimelea vya ukungu wa aina hii huishi kwenye udongo.

Mimea inayoshambuliwa au kuhifadhi ugonjwa huu ni mingi mno na husababisha mnyauko wa miche ya mazao mengi shambani. Mmea uliopatwa na ugonjwa huu huwa mwembamba sanamithili ya waya hasa kwenye shina. Mara nyingine ugonjwa wa aina hii huozesha mche hata kabla ya mche kustawi vizuri.




**Picha namba 10: Ugonjwa wa kinyaushi**

## Ugonjwa wa Ubwiri Poda (Powderymildew)

Ugonjwa huu huenea zaidi vipindi vya joto/ukame. Ugonjwa huu hushambulia zaidi mazao kama Zabibu, nyanya, hoho n.k. Majani huwa na madoadoa ya njano ambayo huambatana na poda nyeupe chini ya jani.



**Picha namba 11: Namna majani ya mizabibu yalivyoathiriwa na fangasi, namna poda nyeupe inavyoonekana katika picha**

## Ukungu wa kuchelewa (Lateblight)

Huu ni ugonjwa wa Zabibu pia ambao kama haukudhibitiwa husababisha madhara kiasi cha karibu asilimia 90-100 ya mavuno. Ugonjwa huu husababishwa na vimelea vya ukungu jamii ya Phytophthorainfestans ambayo hutokea zaidi vipindi vya baridi kali na mvua.

Hayo ni baadhi tu magonjwa ya fangasi, orodha ni ndefu kidogo. Tutajitahidi kuchagua yenye athari kubwa na yanayoshambulia mazao mengi.




**Picha namba 12:** Ukungu wa kuchelewa

Namna ugonjwa huu unavyoweza kuleta madhara kwenye matunda ya mzabibu

Jinsi ya kupambana na magonjwa ya fangasi:

1. Hakikisha unatembelea shamba lako mara 3 hadi 4 kwa wiki, au ikiwezekana kila siku. Unatakiwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, hakikisha unazunguka shambani, kagua mimea yako kwenye majani juu na chini pamoja na shina. Uchunguzi wa mara kwa mara utasaidia kujua kwa haraka dalili za ugonjwa kabla ya kuleta madhara.

2. Hakikisha usafi wa shamba lako kuanzia wakati wa upandaji hadi baada ya kuvuna. Hakikisha palizi inafanyika kwa wakati, maana baadhi ya magugu hutumika kama mazalia ya vimelea vya fangasi, pia magugu shambani husababisha unyevunyevu ambao hustawisha fangasi. Na si hivyo tu magugu pia

huficha wadudu ambao ni waharibifu kwa mimea lakini pia wadudu hao hutumika kusambaza magonjwa hayo ya fangasi

3. Piga dawa kwa wakati hasa katika kipindi cha masika, na hakikisha unatumia dawa sahihi. Mbali na magonjwa hayo ya fangasi pia kuna magonjwa yanayosababishwa na wadudu, kama nzi, mbung'o, funza wa vitumba n.k

Kubaini mapema mayai au funza kabla hayajatoboa matunda ni muhimu sana. Funza wachanga kwanza hula majani baadae matunda. Funza wakishaingia ndani ya matunda husababisha uharibifu mkubwa. Uharibifu kwenye matunda machanga husababisha kupukutika kwake, wakati mashambulizi ya matunda yaliyokomaa husababisha matundu ambayo huruhusu kuingia kwa aina nyingine za ukungu na bakteria ambao huleta madhara zaidi.

Namna ambayo funza hawa wanaweza kuharibu mmea na matunda ya zabibu

Kemikali: Mara nyingi kemikali inayodumu kwa muda mfupi ndio inayohitajika kwani matunda hushambuliwa muda mfupi kabla ya kuvuna.

Kwa hivyo, kemikali kama vile mevinphos na endosulfan zinashauriwa kutumika. Kemikali nyingine zilizosajiliwa kutumika kwa mdudu huyu ni carbaryl, tetrachlorvinphos, methomyl, acephate, monocrotophos na dawa zenye pareto.

Hayo ni baadhi tu ya magonjwa yanayoshambulia Zabibu, ila yapo mengi sana,mpaka wataalam waliamua kuandika kitabu kinachohusu magonjwa tu ya mizabibu,kwa kuwa ndio kiini cha mkulima kuweza kupata mazao mengi kama ataweza kukabilina na magonjwa hayo.

11. Baada ya Zabibu kutoa matunda, kinachofuata ni uvunaji wa Zabibu, katika kipindi kuna hatua kama mkulima inabidi uzitilie mkazo kabla ya kuanza uvunaji, kama kuangalia kiwango cha sukari, ukubwa wa matunda, rangi ya matunda n.k. kwa mzabibu mpya inachukua miezi nane ndio huanza kuzaa japo mzao wa kwanza unakua hafifu, inapofikia miaka mitatu ndipo uzao wake huongezeka maradufu, hivyo kwa anae anza kilimo hiki asije kukata tama kwa kupata mazao machache kwa uzao wa kwanza.

Vifaa vinavyohitajika kwa uvunaji ni mikasi, kisu, kreti/ndoo, japo Wakulima wengi wamekuwa wakitumia viwembe kitu ambacho haishauriwi kwa kuwa ni hatari hata kwa mvunaji mwenyewe.



**Picha namba 13:** Vifaa kwa ajili ya uvunaji Zabibu

Muda wa mzuri wa kuvuna Zabibu ni asubuhi kwa kuwa muda huu jua linakua sio kali, hivyo itasaidia kupunguza matunda mengi kuanguka chini wakati wauvunaji, na pia mvunaji atakua akivuna kwa utaratibu bila kero yoyote ya jua.

Tunashauri wakati kuvuna mtu avune mstari kwa mstari na sio kuvuna hovyo hovyo, ukivuna kwa mstari itasaidia kujua unapoelekea bila kuacha Zabibu zingine shambani, mtu akivuna bila kufuata mstari anaweza kuacha baadhi ya sehemu hazijavunwa kwa kua hajui alianzia wapi na anaelekea wapi, pia atatumia muda mwingi shambani.

Namna watu wanavyovuna kwa mstari, hii inasaidia kuvuna Zabibu yote bila kuacha hata moja shambani

## MWISHO

Kama ilivyoelezwa hapo awali kijitabu hiki sio cha mtaala wa kilimo (academic), bali ni muongozo wa kumuwezesha mkulima wa Zabibu katika kufikia malengo yake hasa kuinua kipato chake kupitia kilimo hiki cha Zabibu.

Ukibahatika kutembelea baadhi ya Wakulima na mashamba yao utaona kuwa kwa asilimia kubwa Wakulima wengi hawalimi kibiashara kilimo hiki bali wanalima ili wapate pesa ya kujikimu tu kama kula na kuvaa basi. Utakuta kuwa Wakulima wengi hawatunzi kumbukumbu za gharama walizoingia katika kulihudumia shamba lake hivyo pia inakua ngumu kujua kama wanapata faida kiasi gani. Hivyo mkulima anahimizwa kutunga kumbukumbu na kufuata miongozo ya aina hii ili kujiletea tija katika uzalishaji wa Zabibu.

## Bibliografia

Kijitabu hiki kimeandaliwa na kutafsiriwa kwa kurejea bibliografia zifuatazo:

Creasy, G. L., & Creasy, L. L. (2009). Grapes: Crop production science in horticulture. Oxfordshire, United Kingdom: CABI.

Carisse, O. et al. (2006). Identification guide to the major diseases of grapes. Agriculture and Agri-Food Canada publication. http://www.agr.gc.ca/resources/prod/doc/sci/pub/pdf/id_guide_major_diseases_grapes_e.pdf

Fahey, D. (2015). Grapevine management guide. New South Wales Department of Primary Industries publication. http://www.dpi.nsw.gov.au/__data/assets/pdf_file/0017/302840/12968-Grapevine-mment-guide-2014-15-web-ver.pdf

FAO. (2009). Agribusiness handbook – grapes, wine. United Nations Food and Agriculture Organization. http://www.fao.org/docrep/012/al176e/al176e.pdf